

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)

Nambari ya Simu 023 2401045

Email: ded.kisarawed@pwani.go.tz



Sanduku la Posta 28001,
Kisarawe,
PWANI.

Tarehe: 14 Februari, 2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe anapenda kuwatangazia nafasi za Ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la Anwani za Makazi katika Kata na Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

A. SIAFA ZA WAOMBAJI

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 – 35.
- ii. Awe na Elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- iii. Awe anamiliki simu janja Android yenyewe uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- iv. Awe na barua pepe (email) na nywila (password) inayofanya kazi.
- v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za Vijiji.

B. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- iii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za Makazi.
- iv. Kutuma data kwenye mfumo wa anuwani za makazi.

C. MAOMBI YAAMBATISHWE NA;

- i. Nakala ya Cheti cha kidato cha nne na kuendelea.
- ii. Nakala ya Cheti cha kuzaliwa.
- iii. Picha (Passport size 2).
- iv. Barua ya maombi ipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji alipo muombaji.
- v. Hakikisha unataja namba zako za simu ya mkononi.

D. MALIPO


Malipo yatafanyika kwa kiasi cha kazi kwa siku.

E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba za simu, barua pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata alipo muombaji kwa kutumia anuani ifuatayo: Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, S.L.P 28001, **KISARAWE**.

F. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 22/02/2022 saa 9:30 Alasiri.


James C. Chitumbi
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

